# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE FOURTEEN: “Doing It Right”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: LINDA CALLS HER MOTHER FROM HER MOBILE**

- **Linda (f, 20)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**

**SCENE TWO: CHIVASI WORKING ILLEGALLY AS A GARDENER**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Ralph (m, 40)**

**SCENE THREE: CHIVASI AT RHODA'S HOUSE**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Rhoda (f, 25)**

**SCENE FOUR: FARAHANI IS GRANTED ASYLUM**

- **Farahani (m, 19)**
- **Immigration officer (m, 40)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hii ni sehemu ya 14 katika mchezo huu wa Redio **“Ardhi ya Ahadi,- hadithi kuhusu Wahhamiaji wa Afrika Barani Ulaya”**, ambapo tunaangzia sababu zinazowafanya Waafrica wengi kuhamia Ulaya, na changamoto wanazopitia.Katika kipindi kilichotangulia Chivasi anashindwa kuwashawishi maafisa wa uhamiaji katika mahojiano ya ombi lake la kutaka kupewa hifadhi kama Mkimbizi Ulaya. Hatimaye anafanikiwa kutoroka kambi ya kuzuizi wanakozuiliwa wahamiaji bandia baada ya kushauriwa na Farahani kujificha chini ya rada ili kuendelea kuishi Ulaya. Chivasi anafanikiwa kutoroka na kufika kati kati mwa mji wa Ulaya, ambako anakutana na Rhoda anayemsaidia. Huku hayo yakijiri, Florence na Charles wanatiwa nguvuni kwa tuhuma za kuhusika kwenye sakata ya kupanga Ndoa bandia, na kumuacha Linda asijue la kufanya.. wahusika wetu wakuu kwenye mchezo huu wamo mashakani. Je hii ndiyo hali inayowakumba wahamiaji wote? Ni vipi wanaweza kujinasua na kuishi maisha bora huko Ulaya. Haya ndiyo tunayoangazia katika kipindi cha leo **“Tenda Haki”.** Na moja kwa moja tunaanza na Linda ambaye anahangaika kupiga simu.

**SCENE ONE: LINDA CALLS HER MOTHER FROM HER MOBILE**

1. **SFX: BEEPING SOUNDS OF DIALLING ON A MOBILE PHONE**

2. **LINDA:** **(nervous)** Mama chukua simu. …Tafadhali chukua simu Mama….

3. **MRS. MARAGA:** **(sleepy voice)** Hello? Linda – Una nini binti yangu?. Sasa hii ni usiku wa manane hapa.

4. **LINDA:** **(breaks down in tears)** Mama… Mimi.. Ni...

5. **MRS. MARAGA:** **(fully awake)** Linda! Kuna tatizo? Una tatizo gani?. Kumetokea nini?

6. **LINDA:** Siwezi kuendelea na maisha haya Mama. Nataka kurudi nyumbani. Nataka kurudi…!

7. **MRS. MARAGA:** Nisikize Linda..Kama ni kuhusu Babako, usijali Madaktari wanasema atappona baada ya kufanyiwa oparesheni. Hivyo hakuna haja ya kuwa na hofu ya kutaka kurudi nyumbani. Na unafahamu kwamba hatungeweza kugharamia matibabu kama isingekuwa kupitia msaada wako.

8. **LINDA:** Mama nafurahi sana kusikia hali ya Baba anavyoendelea. Lakini hii haihusiani kamwe na Baba..

9. **MRS. MARAGA:** Inahusiana na nini tena. Au unatamani nyumbani? Haiwezekani kwamba unatamani nyumbani mara moja hii , umekuwa hapa hivi majuzi tu na tuliona mambo yanakwendea vizuri huko Ulaya.…

10. **LINDA:** Mama samahani kwa kukusumbua wakati huu wa usiku. Tafadhali samahani sana… .

11. **MRS. MARAGA:** **(concerned)** Linda-, Kwani umefanya nini? hebu niambie Binti yangu! Mimi ni Mamako.. Hata kama umepata mimba nitakusaidie!. Usijilaumu na kufanya mambo yasiyofaa.

12. **LINDA:** Hata sina mimba mama.… Mama samahani sana., siwezi kukuambia haya kwenye simuI… Kwaheri. Usiku mwema na umsalimie sana Baba.

13. **MRS. MARAGA:** Linda, subiri!

14. **SFX: CALL DISCONNECTED WITH A BEEP**

15. **NARRATOR:** Mamake Linda amebaki akishangaa baada ya Linda kukata simu. Anajaribu kumpigia lakini hakuna mti anayejibu. Bi Maraga anagagaa kitandani ausiku mzima kwa kukosa usingizi. Ana wasi wasi kwamba lazima binti yake amepatwa na matatizo. Lakini ni matatizo gani yaliyompata Binti yake? Anaomba tu kwamba Binti yake ataweza kukabiliana na matatizo hayo. Lakini sasa hebu tumgeukie Chivasi. Bada ya kutoroka kuzuizini anaokolewa na Rhoda. Msamaria mwema ambaye anakubali kumsaidia. Na baada ya kuondoka nyumbani kwa Rhoda Chivasi anashindwa atakwenda wapi!.Hana pesa na kwa muda wa siku kadhaa anabaki akilala vibarazani ,kewnye vituo vya gari

moshi na kwenye bustani pamoja na watu wengine wasio na makao. Siku moja, mwenzake pia asiye na makao, anamsadia kupata kibarua cha kutunza bustani ya maua ili aweza kujipatia pesa kidogo za matumizi. Chivasi anafanya kazi kwa Bwana Ralph ambaye anakubali kumlipa kila mwisho wa wiki. Hebu sasa tuungane na Chivasi akiwa kibaruani.

**SCENE TWO: CHIVASI WORKING ILLEGALLY AS A GARDENER**

16. **SFX: ELECTRIC HEDGE TRIMMER TRIMMING A BUSH / BIRDS OUTSIDE**

17. **RALPH:** **(angry)** Wewe! Wewe! unafanya nini?

18. **SFX: ELECTRIC HEDGE TRIMMER SWITCHED OFF**

19. **RALPH:** Nimekwambia uzichane vizuri sehemu za pembeni ziwe ndogo. Sasa angalia ulivyofanya! Majirani na wapiti njia wote wataweza kunichungulia dirishani kwangu.

20. **CHIVASI:** **(polite)** Lakini bosi… , nimejaribu kuchana maua kama ulivyoniagiza. Sio juu na sio chini sana!.

21. **RALPH:** Nini? Unasema niini?! Unataka kuniambia kwamba sikumbuki nilivyokuagiza? Nyinyi waafrica hamuelewi mambo haraka. Muna vichwa vigumu sana. Samahani lakini siwezi kukulipa pesa zako Umeharibu bustani yangu.

22. **CHIVASI:** **(protesting)** Hapana ! Huwezi kufanya hivyo!

Nimekufanyia kazi kwa zaidi ya masaa kumi kila siku kwa muda wa wiki moja iliyopita. Na nimefanya kulingana na maagizo yako. Lazima utanilipa pesa zangu kama tulivyokubaliana.

**23. RALPH:** Ohh, sasa unanitisha? Na ni makubaliano gani hayo unayozungumzia? Sielewei unasema nini!. Hakuna mkataba wowote tuliofikiana , na ukisisitiza nikulipe kwa kuniharibia bustani yangu ya maua, basi nitaenda polisi kukushtaki kwa kufanya kazi hapa bila ya kibali.

**24. CHIVASI:** Nimefanya kazi kwa bidii sana katika bustani hii yako Ralph, nina haki ya kulipwa pesa zangu.

**25. RALPH:** Sawa, umeshinda! Hebu niwaite mafiasa wa Polisi. Wewe utarejeshwa nyumbani Afrika!

**26. SFX: ELECTRIC TRIMMER SWITCHED ON AGAIN**

**27. RALPH:** Unafanya nini sasa? hebu weak chini! **(screaming in fear)** Nisaidieni!

**28. SFX: SOUND OF FEET RUNNING AWAY, CRIES FADING**

**29. NARRATOR:** Chivasi anapunguza hasira. Na baada ya kupata fahamu zake, anajuta kwanini alijaribu kuchukua sheria mikononi na kutaka kumshambulia mzungu. Mbona ulimwengu umebadilika ghafla? Matatizo anayopitia ni dhihirisho kamili la ugumu wa maisha tangu ahamie Ulaya. Kwa uoga Chivasi anaamua kutorokea nyumbani kwa

Rhoda. Na kufinya kengele ya mlango kwa nguvu.

**SCENE THREE: CHIVASI AT RHODA'S HOUSE**

30. **SFX: RINGING ON DOORBELL SEVERAL TIMES**

31. **RHODA:** **(answers through entryphone)** Ni nani ? Kwanini unafinya kengele jinsi hiyo?

32. **CHIVASI:** **(panting)** Rhoda, ni mimi Chivasi. Tafadhali nifungulie.

33. **SFX: BUZZING OF ENTRYPHONE AND DOOR BEING PUSHED OPEN**

34. **RHODA:** Chivasi! Kuna nini? Ni kana kwamba umekuwa ukikimbia mbio za Marathon.

35. **CHIVASI:** Rhoda, Nimefanya ujinga sana! Najijutia.. Nimetoroka na sikuwa na mahali kwengine kwa kukimbilia usalama wangu…. isipokuwa hapa kwako!

36. **RHODA**: Kuna tatizo? Kumetokea nini?

37. **CHIVASI**: Nimekuwa nikifanya kazi nyumbani kwa Mzungu mmoja kwa muda ya wiki moja sasa, na amekataa kunilipa pesa zangu! Nimekasirika… na kutisha kumshambulia. Hata hivyo sikumjeruhi lakini.

**RHODA:** Sawa. Sikiliza Chivasi! Hebu nielezee kuhusu historia ya maisha yako, kwasababu wakati nilipojaribu kukusaidia mara ya kwanza hukutaka kuzungumza chochote. Unashida gani? Wewe ni mtoro? Umetenda uhalifu wowote? Au umehamia Ulaya bila kibali?

**38. CHIVASI:** **(catches breath)** Ndiyo, nime.. nimehamia Ulaya kutoka Afrika baada ya kudandia meli. Na wakasema watanirudisha kwetu Afrika. Ndio sababu nikatoroka kizuizini.

**39. RHODA:** Kwanini ? Kwanini kuhatarisha maisha yako ? Sielewi!

**40. CHIVASI:** Huelewi nini? Kila mmoja anafanya hivi! Kwani wewe umefikaje Ulaya? Umezaliwa hapa?

**41. RHODA:** **(laughs)** Hata mimi sikuzaliwa hapa! Nimekuja hapa kama mfanyi kazi wa nyumbani ambaye ajira yake ni chakula na mavazi yaani “***Au pair”*** Nilipomaliza masomo yangu ya chuo kikuu nilijisajili na shirika la kuwatafutia watu kazi za nyumbani, na baada ya muda wa wiki chache nilijikuta hapa Ulaya.

**42. CHIVASI:** **(surprised)** Kweli? Kwa hivyo mimi pia ningefuata utaratibu huo ningeepukana na mashaka haya yote?

**43. RHODA:** Sidhani kama shirika hutoa ajira kwa wanaume, lakini lazima kuwe na mashirika mengine yanayotoa huduma za aina hiyo hasa kwa watu wenye taaluma. Hata hivyo nilikuwa na bahati kwa sababu muajiri wangu hapa ni mtu mkarimu sana. Wananichukulia kama mmoja wao, na hata kunihimiza kusoma hapa. Kuishi nao kumenisaidia kukuza lugha yangu wakati nilipoanza kuishi nao kumenisaidia sana kupata uzoefu wa kuzungumza lugha ya hapa na hivyo kutangamana na watu kwa urahisi, kufanya urafiki na hatimaye kuendelea na masomo yangu ya chuo kikuu.

**44. CHIVASI:** Una bahati sana! Kama ningefahamu kuwa ni rahisi kupitia mpango huo, ningekuwa nimemueleza Linda.

**45. RHODA:** Linda? Ni dadako?

**46. CHIVASI:** Usijali.. hebu endelea…

**47. RHODA:** Baada ya kufuzu chuo kikuu, nilipata kazi kama mtaalam wa madawa na kupata kibali cha kufanya kazi hapa. Tangu hapo nimekuwa nikiishi hapa na kuisaidia familia yangu nyumbani.

**48. CHIVASI:** Hivyo ni vizuri sana! Je una mipango ya kurudi nyumbani. Naona umefanya makazi hapa kwa

muda murefu, lakini hujaolewa.. sivyo?

**49. RHODA:** Sijaolewa! Ila ninaye Mchumba ambaye anafanya kazi na kuishi Afrika. Tunapanga kuoana mwishoni mwa mwaka huu. Hapo ndipo tutaamua ni wapi tunataka kuanza maisha yetu ya familia.

**50. CHIVASI:** Rhoda, nashukuru sana kwa yote uliynifanyia. Umekuwa mkarimu sana kwangu. Sijui kama naweza kukuomba msaada mmoja tu…? Mimi nimekuwa nikifanya kazi katika shamba la huyu mzungu kwa muda wa wiki moja ili kupata nauli ya gari moshi kuelekea Jijini. Lakini muajiri wangu amekataa kunilipa mshahara na sina pesa zozote sasa! Unaweza kunisaidia na pesa kidogo? Najua si vizuri kuomba omba, lakini nahitaji sana kufika huko. Nataka kwenda chuo kikuu.

**51. RHODA:** Kweli. Unajua mara nyingi nakutana na watu wanaoniomba Pesa kunilaghai. Lakini wewe naona unasababu nzuri sana Chivasi. Naamini kwamba ni mtu mzuri. Lakini sijui kwanini ukaamua kuhatarisha maisha yako kuja hapa, lazima iwe ni sababu muhimu sana.

**52. SFX: DRAWER BEING OPENED**

**53. RHODA:** Shika hizi yuro mia moja . Nafikiri zitakutosha kukupeleka unakotaka kwenda.. .Na hizi ni nambari

zangu za simu nipigie wakati wowote unapohitaji msaada.

54. **CHIVASI:** Ahsante sana . Sijui nitakulipa vipi.

55. **RHODA:** Usijali Chivasi. Chivasi. Kuanzia leo kila kitu unachotaka kufanya lazima ufuate utaratibu na sheria. Hilo litakusaidia.

56. **CHIVASI:** Nitakumbuka ushauri wako. Niombee nifike bila kukamatwa na maafisa wa uhamiaji . Kuna Mtu nahitaji kukutana naye. Mtu muhimu sana maishani mwangu.

57. **NARRATOR:** Baada ya Rodha kumpa pesa hizo, bila kupoteza muda Chivasi anakwenda moja kwa moja hadi kituo cha gari moshi ambako anakata tikiti kuelekea mjini ambako Linda anasomea Chuo kikuu. Katika kambi ya kuzuizi, uamuzi umetolewa kuhusu ombi la Farahani kupewa hifadhi kama mkimbizi. Je hii inamaana ndoto yake ya kuishi maisha mazuri imetimia?. Endelea kusikiliza. Listen on.

**<u>SCENE FOUR: FARAHANI IS GRANTED ASYLUM</u>**

58. **SFX: FILE BEING OPENED**

59. **IMM. OFFICER:** Farahani,niko na habari njema. Baada ya kuchunguza kwa makini ombi lako, hatimaye idara ya uhamianji imekubali upewe hifadhi kama mkimbizi. Hizi ni stakabadhi za kukutambua ramsi kama mkimbizi nchini mwetu. Unajisikiaje sasa?

60. **FARAHANI:** **(choking with happiness)** Asante sana. Nashukuru sana!. Hii ni muhimu sana kwangu!. Sasa naweza kwenda kuanza kufanya kazi?

61. **IMM. OFFICER:** Si haraka hivyo kijana . Huu ni mwanzo tu.Hebu subiri nikieleze utaratibu wa kuomba ukimbizi humu nchini. Utapewa huduma na mahitaji yako kama mkimbizi, kukuwezesha kuishi maisha ya kawaida. Hutaruhusiwa kuondoka kambi ya wakimbizi. Lazima ufuate sheria zote katika kambi hiyo ya wakimbizi. Serikali itakupa chakula, makaazi na pesa kidogo za matumizi. Unaweza kupewa pesa taslimu au hati ya malipo yaani “*Vocha*” ambayo unaweza kuitumia kununua chakula. Haruhusiwi kufanya kazi ya malipo ukiwa katika kambi ya wakimbizi. Endapo utapatikana ukifanya kazi basi utapokonywa haki yako ya ukimbizi. Tumeelewana?

62. **FARAHANI:** **(dumbfounded)** Ah… ah… Sijakuelewa vizuri.., unaweza kurudia sehemu ya mwisho ...

**OUTRO:**

Na hadi hapo ndipo tunafika mwisho wa sehemu hii ya 14 ambapo Farahani ameshangazwa na ukweli wa mambo kuhusu hali ya wakimbizi Ulaya. Linda naye hana habari kwamba Chivasi yuko hatua chache tu kufika chuo kikuu anakosomea. Je nini kitakachotokea akimshtukizia mlangoni? Usikose kuungana nasi katika sehemu ya mwisho kwenye mchezo huu kuhusu Waafrica wanaohamia Ulaya.Nini maoni yako? Je unadhani sheria katika

kambi za wambizi huko Ulaya ni haki au ni ukandamizaji? Ungana nasi kwenye sehemu ya mwisho ya mchezo huu na tungependa kupata hoja zako kuhusiana na sauala zima la Waafrica wanaohamia Ulaya kihalali na kufanikiwa kimaisha. Pia ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki usisite kutembelea mtandao weu wa dw-de/destinationeurope. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.